TANGAZO LA SERIKALI Na. 102 la tarehe 16/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEOLA MWELA, KITONGOJI CHA LUSUNGO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Katika Eneo la Mwela, kitongoji cha Lusungo ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

*Tangazo la Serikali Na.102 (Linaendelea.)*

———

JEDWALI

———

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 58739MS, 88989101KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki mwa kituo cha Afya Mwakaleli katika uelekeo wa KS 69$^0$ 49' 02.27 MS kwa umbali wa kilomita 1.27 hadi kwenye alama ya mpaka namba B yenye majira-nukta 586936MS, 8988661KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ13$^0$ 40' 16.71MS kwa umbali wa kilomita 0.04 hadi kwenye alama ya mpaka namba C yenye majira-nukta 586945MS, 8988698KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ 77$^0$ 37' 09.28MS kwa umbali wa kilomita 0.08 hadi kwenye alama ya mpaka namba D yenye majira-nukta 587027MS, 8988716KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa wa KS 82$^0$ 04' 02.07.28MS kwa umbali wa kilomita 0.61 hadi kwenye alama ya mpaka namba E yenye majira-nukta 587637MS, 8988631KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea KusiniMashariki katika uelekeo wa KS 47$^0$ 57' 39.37MS kwa umbali wa kilomita 0.08 hadi kwenye alama ya mpaka namba F yenye majira-nukta 587698MS, 8988576KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS 6$^0$ 41' 46.96 MS kwa umbali wa kilomita 0.25 hadi kwenye alama ya mpaka namba G yenye majira-nukta 587727MS, 8988329KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS 53$^0$ 50' 30.53 MG kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi kwenye alama ya mpaka namba H yenye majira-nukta 587649MS, 8988272KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea KusiniMagharibi mwa mto Mwantisi katika uelekeo wa KS 85$^0$ 58' 18.25 MG umbali wa kilomita 1.64 hadi kwenye alama ya mpaka namba I yenye majira-nukta 586016MS,8988157;baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi mwa Kijiji cha Lugombo katika uelekeo wa KZ 16$^0$ 21' 12.19MG umbali wa kilomita 0.98 hadi kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 585739MS, 8989101KZ unapoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*